

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
Tarehe 17 Novemba 2007**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Mussa Omari
Paulo Atibu Hatibu
Protace Mugondo
Sudi Saidi Ramadhan

Siku ya uamsho wa mabadaliko ya majira

Wakati wa wiki Venant alitafsiri barua kuhusu mabadaliko ya majria na Damas alisahihisha na alitumia Elaine kwa email. Wanachama walisoma barua kwa kiswahili na hawakubadalisha. Venant na Damas hawakuweza kuja kwenye mkutano huu. Damas bado hajatupa orodha ya mashirika wataosaini barua lakini alisema kwa simu kwamba ataendelea kufuatilia wiki hii. Ally Saidi Mohammad, Juma na Protace wote walisema watajaribu kupata jina kamili na contacts za mashirika ya mazingira wiki hii. Wanachama walikubali kumwomba Sosthenes kutengeneza mabango. Elaine alisema atawasiliana na ofisi ya Makamu Rais na Ubalози wa Merekani kuwapa taarifa ya tukio na kuomba mtu wa kutupokea barua zetu siku yenyewe.

Msafara wa Baisikeli

Juma aliwapeleka repoti ya msafara Mbunge Azzan Zungu, Kampuni ya Guta, Kampuni ya Bakhresa na Ubalози wa China wakati wa wiki. Alitumia Tsh 5,000 kwa ajili ya photocopy pamoja na photocopy ya rangi ya picha.

Ubalози wa Uholonzi bado hawajalipa hela ya udhamini inayobaki.

Halmashauri ya Jiji

Tuna nakala moja ya michoro ya mradi ya DART, basi Ally Saidi Mohammed alisema atatoa photocopy wiki hii kuacha ofisini ili wanachama wasome.

Mawazo wetu wa mwanzo :

- Kwa ujumla michoro yanatoa kupau mbele kwa wapanda baisikeli
- kwenye stretch 2 na Mtaa Msimbazi ambapo hakuna sehemu ya njia ya baisikeli, tuulize wapanda baisikeli, maguta na baisikeli za walemevu waende kwenye barabara kubwa au sehemu ya watembea kwa miguu
- kwenye stretches zote tupate taarifa wapi maguta na baisikeli za walemavu waende na kama kuna upana wa kutosha
- kwenye stretches zingine kuna sehemu kati ya barabara kubwa na njia ya baisikeli lakini kwenye stretches zingine hakuna. Tupate taarifa kuna nini sawa sawa kwenye sehemu hii (miti, drains) na vipi wapanda baisikeli tutalindwa kama hakuna sehemu hii.
- Tunahitaji taarifa kuhusu vipi magari yataingia kwenye plots na kama wataweza kuingia sehemu ya baisikeli kupaki au kwenda mpaka plot

Ofisi, guta na mambo ya hela

Wakati wa wiki Juma na Elaine walichukua Tsh 44,000 kutoka benki na Juma alimpa Ally Saidi Mohammad Tsh 50,000 ambaye atatumia kununua bao laini kwa bao za tangazo. Bado hajafanya kazi hii.

Violeth ambaye anatafsiri dondoo amempa taarifa Elaine kwamba anakaribia kumaliza.

Kampuni ya guta walimwambia Juma kwamba spea za guta bado zipo bandarini lakini zitapatikana tarehe 20. Jumanne alimpa Juma Tsh 14,000 kama hela za nyuma za kukodi guta na hatuchukui hela kwa wiki ambapo guta haifanyi kazi, basi hela yote imelipwa mpaka sasa. Jumanne alipendelea Ally Saidi Mwishehe awe dereva mpya wa guta wakati spea zinaingia.

Juma sasa ana Tsh 92,000 ya hela ya UWABA na balance ya benki imefika mpaka balance ya chini ya Tsh 2,000.

Mchango wa Italia imefika National Microfinance Bank lakini bado haijawekwa kwenye akaunti ya UWABA kwa sababu ya machanganyikio. NMB walisema watafuatalia kupata taarifa sahihi kwamba ni hela yetu na Elaine alimtumia email kwa David wa Bike Nouveau Italy kumwoba atoe taarifa sahihi kwa benki yake kwamba hela ni kwa ajili yetu.

Wamba memorial fund bado hawajajibu email kuhusu mradi wa usalama barabarani. Elaine atawapigia simu wiki hii.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji

Bwana Wemba bado hajajibu barua yetu ya kuomba semina ya usalama barabarani.

Maoni

Protace alipendekeza kwamba UWABA atoe ajira kwa mtu kufanya kazi ya kila siku ya ofisi. Wanachama walieleza kwamba Jumanne ana ofisi yake jirani na pia Ally Saidi Mohammed anakaa jirani basi kawaida wao wanawasiliana na mtu yeyote anayefika ofisini kwetu. Juma, Elaine na wanachama wengine wanafanya kazi za utawala kwenye muda wao wa spare time. Aidha hatuna hela ya kutosha ya kuwa na ujibu wa kumpa mtu ajira ya kila siku. Elaine alisema kwamba kama tunapata hela ya kutosha baadaye ni bora tumpe ajira mtu ambaye tayari ameshafanya kazi sana za UWABA na ambaye yupo tayari kufanya kazi hii.

Nyingenezo

Tuliongea sana kuhusu neno moja iliyotumikwa na Protace wakati wa kutoa maoni – neno la “Chama” na “Umma” na lugha inayoonyesha UWABA ni kundi ya wanachama na siyo viongonzi tu.

Paulo alifanya lamination ya vitambulisho wakati wa wiki na aliwapa wanachama.